THE SALVATION ARMY

SIKU YA KIMATAIFA

KUA

YA WATOTO NA VIJANA 2024

MUHTASARI WA MADA

UTANGULIZI

Karibu kwenye kiini cha ‘KUA’ ! Maandishi haya yanahusu kukua na maana yake nini kwetu sisi Wakristo. Unaona, kukua ni sehemu muhimu ya maisha yetu. Inahusu kuwa mwerevu zaidi, mwenye nguvu zaidi, na mwenye upendo zaidi tunapomfuata Mungu na kujifunza zaidi kuhusu yeye.

Description automatically generatedNdani ya maandishi haya, utakutana na vifungu vya Biblia vinavyozungumzia ukuaji. Vinatuonyesha tunahitaji nini ili tukue kiroho, tunaweza kukua namna gani, na namna gani Mungu ataujenga Ufalme wake. Inastaajabisha kuona jinsi ukuaji unavyoweza kutupa mguso mkubwa katika maisha yetu na dunia inayotuzunguka!

Kwa kweli tunatumainia hiki kiini cha “KUA” kitasaidia na kitaleta furaha kwako. Lengo lake ni kuhamasisha, kikufanye ufikiri, na uanzishe mazungumzo kuhusu ukuaji na marafiki zako na familia yako. Tunaposafiri pamoja katika safari hii, hebu tufungue mioyo na akili zetu kwa hekima ya Biblia. Inaweza kutusaidia kwa sababu watu wa Mungu wa ajabu wanatutaka tuwe hivyo.

Kwa hiyo, tuwe na furaha tunapochunguza na kugundua mambo yote ya kipekee yanayohusu ukuaji! Inaweza kufanya mambo ya kipekee maishani mwetu na kutusaidia kutimiza mpango maalum wa Mungu kwetu.

VIFUNGU VYA BIBLIA VINAVYOONYESHA UKUAJI

*‘Wenye shina na wenye **kujengwa** katika yeye, mmefanywa **imara** kwa imani, kama mlivyofundishwa, mkizidi kutoa shukrani.*

- Colossians 2:7 (NLT)

Kama mti unavyohitaji mizizi imara ili ukue mrefu na uzae matunda, sisi vile vile tunahitaji kujikita. Upendo wa Mungu na kweli yake ndivyo virutubisho vyetu katika kila sehemu ya maisha yetu. Kwa kukumbatia upendo wa Mungu na kazi yake iletayo mabadiliko ndani yetu, kupitia kwa Roho Mtakatifu, tutakua katika maisha yanayotosheleza na yenye kusudi. Na matokeo ya mwisho? Tutabubujika shukurani!

‘Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa Mbinguni umefanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake, nayo ni ndogo kuliko mbegu zote, lakini ikiisha kumea, huwa kubwa kuliko mboga zote, ikawa mti, hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake.”

Mathayo 13:31-32

Yesu aliutoa mfano wa mbegu ya haradali kuonyesha jinsi ufalme wa Mungu unavyoweza kukua. Hadithi hii ndogo inatuonyesha kwamba mianzo midogo inaweza kusababisha upanuzi mkubwa. Vile vile kama mbegu ya haradali, imani yetu, matendo na michango yetu midogo inaweza kuwa na nguvu ya kuleta mguso mkubwa na mabadiliko katika dunia hii.

Baada ya hayo Yesu alikwenda zake ng’ambo ya Bahari Galilaya, nayo ndiyo ya Tiberia. Na mkutano mkubwa wakamfuata, kwa sababu waliziona ishara alizowafanyia wagonjwa. Naye Yesu akakwea mlimani, akaketi huko pamoja na wanafunzi wake. Na Pasaka sikukuu ya Wayahudi, ilikuwa karibu.

Basi Yesu alipoinua macho yake akaona mkutano mkuu wanakuja kwake, alimwambia Filipo, tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula? Na hilo alilinena ili kumjaribu, kwa maana alijua mwenyewe atakalotenda. Filipo akamjibu, Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi kila mmoja apate kidogo tu.

Wanafunzi wake mmoja wapo, Andrea nduguye Simoni Petro, akamwambia, yupo hapa mtoto yuna mikate mitano na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa? Yesu akasema waketisheni watu. Na mahali pale palikuwa na majani tele. Basi watu waume wakaketi, wapata elfu tano jumla yao. Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi, na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka.

Nao waliposhiba, aliwaambia wanafunzi wake, kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote. Basi wakakusanya, wakajaza vikapu kumi na viwili, vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyobakia wale waliokula.

Basi watu wale, walipoiona ishara aliyoifanya, walisema, hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimwenguni. Kisha Yesu hali akitambua ya kuwa walitaka kuja kuumshika ili wamfanye mfalme, akajitenga, akaenda tena mlimani yeye peke yake.”

Yohana 6:1-15
(Kuwalisha watu 5000, vifungu vya msaada)

Uliwahi kufikiri kwamba mtoto mdogo angeweza kuwa chanzo cha muujiza mkubwa wa kulisha watu 5000? Inawezekana hukuwahi kufikiria hivyo. Katika hadithi hii, Yesu anadhihirisha ukweli kuhusu kujitoa na kumruhusu Yesu atumie kile tulicho nacho mkononi: yeye atakizidisha! katika Ufalme wa Mungu, hata vile vidogo vinaweza kusababisha wingi! Je, tuko tayari kuwashirikisha wengine vile tulivyo navyo? Yesu anatupa changamoto naye anaahidi kwamba anaweza kubadilisha ile zawadi ndogo iwe kitu kikubwa mno.

*'Then we will no longer be immature like children. We won't be tossed and blown about Ili tusiwe watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na k**ukua** hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye, mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, **huukuza** mwili upate **kujijenga** wenyewe katika upendo.*

- Waefeso 4:14-16*

Sote twataka kukua, kimwili, kihisia na kiroho. Kifungu hiki cha Biblia kinatusaidia kufahamu kwamba kumtazama Yesu kutasaidia ukuaji wetu kwa kutuhamasisha tuwe zaidi kama yeye. Tunaweza kukua katika upendo wetu na utumishi kwa Mungu na kwa wengine. Lakini ukuaji nao unahusu kazi ya timu. Sisi ni sehemu ya familia ya Mungu na Ufalme wake, hatuko peke yetu. Tunahitajiana ili tukue! Sote tumepewa zawadi maalum ya kutumia katika kuwatumikia na kuwasaidia wengine katika ukuaji wao.

* Kifungu hiki kinatumika vile vile katika mafundisho yanayoitwa 'Kua', ambayo yametengenezwa na Teritori ya Canada na Bermuda. Masomo hayo yanawahusu wasichana wa umri wa miaka 12-17 nayo yapo kwa Kiingereza na Kifaransa. Masomo mengine yanaweza kutumika katika makundi mchanganyiko. Tafadhali, tembelea https://salvationist.ca/womens-ministries/grow/ uone miongozo kwa viongozi, video za mafunzo, na mitaala ya Kua. Masomo hayo ni ya hali ya juu na inastahili uyaone!